

MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI (VETA)

MKATABA WA UJENZI

Mkataba huu umesainiwa leo tarehe 21 mwezi 07 2022

KATI YA

Chuo cha Ufundi Stadi (na Huduma) cha MPANDA, S.L.P. 190,
MPANDA ambacho kinaiwakilisha Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya
 Ufundi Stadi, S.L.P. 2849 Dar es Salaam (ambacho katika Mkataba huu atajulikana
 kama "Mwajiri") kwa upande mmoja;

NA

PASCAL - G. KWIMBA S.L.P. 190, MPANDA.

(ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "Fundii") kwa upande mwengine

KWA KUWA Mwajiri ana mpango wa kujenga Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya
CHUNYA;

KWA KUWA Mwajiri anatumia rasilimali zake za ndani kwa ushirikiano na rasilimali za
 nje kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya CHUNTA;

KWA KUWA Mwajiri amefanya majadiliano na Fundi kwa ajili ya kazi ya
KUSIKIWA, KUPOKA RANGI, KUNWEKA LAKAFU NA VIGOE KIK
MAJENDO YA UYOO NA KIBONDO CHA MLINZI,

NA KWA KUWA Mwajiri amempatia Fundi nakala ya Michoro pamoja na Achanganuo
 wa vifaa vya Ujenzi (*Schedule of materials*) vinayoonesha namna kazi itakavyofanyika;

HIVYO BASI, PANDE ZOTE MBILI ZINAKUBALIANA KAMA IFUATAVYO:

1. GHARAMA YA UFUNDI

Kwamba, kwa gharama ya Shilingi za Tanzania 5,020,000/- Fundi
 atafanya kazi ya VIGOE NA RANGI kwa masharti yaliyo katika Mkataba huu.
 Katika Mkataba huu, kiasi hiki cha fedha kitajulikana kama "Gharama ya Ufundi"

2. MABADILIKO YA GHARAMA YA UJENZI (CONTRACT SUM ADJUSTMENT)

Gharama ya ufundi haitabadilika kwa namna yoyote ile isipokuwa itakapokuwa imeelekezwa moja kwa moja katika Mkataba huu kutokana na mabadiliko ya ujenzi yaliyofanywa na Mwajiri.

3. NAMNA YA KUFANYA MALIPO

Mwajiri atamlipa Fundi kwa hundi ndani ya siku kumi na nne kwa namna ifuatayo;

- (a) Malipo ya awali, 10 % ya gharama ya ufundi
- (b) Kazi ikikamilika kwa asilimia 20: 15% ya Gharama ya Ufundii;
- (c) Kazi ikikamilika kwa asilimia 50: 20% ya Gharama ya Ufundii;
- (d) Kazi ikikamilika kwa asilimia 80:30% ya Gharama ya Ufundii;
- (e) Kazi ikikamilika kwa asilimia 100: 20% ya Gharama ya Ufundii;na
- (f) Baada ya kukamilika kwa "Muda wa matazamio":5% ya Gharama ya Ufundii.

4. MAKABIDHIANO YA ENEO LA KAZI, UKAMILISHAJI WA KAZI NA KUAHIRISHA KAZI

- (a) Fundi atakabidhiwa eneo la tarehe 9 mwezi _____ 2020 au tarehe nyingine kabla au baada ya tarehe tajwa. Iwapo Fundi atakabidhiwa tarehe nyingine kabla au baada ya tarehe tajwa, pande zote zitaweka kumbukumbu kwa maandishi siku ya makabidhiano ambapo pande zote mbili zitasaini.
- (b) Fundi atakamilisha kazi ndani ya siku 9. toka tarehe ya makabidhiano ya kazi hiyo. Iwapo kutatokea mabadiliko ya ujenzi yaliyofanywa na Mwajiri, siku ya ukamilishaji wa ujenzi inaweza kubadilika.
- (c) Mwajiri anaweza kuahirisha kazi zilizo katika Mkataba huu na kutoa maelekezo kwa Fundi kuhusiana na kuahirisha kazi hiyo.

5. WAJIBU WA FUNDI


Fundi atakuwa na wajibu ufuatao: -

Kujenga Ranzu na Kusandika Vigae

- (a) Kujenga _____ na kukamilisha ujenzi kama inavyoonekana katika Michoro pamoja na Mchanganuo wa Vifaavya Ujenzi (*Schedule of materials*) sambamba na maelekezo ya Mwajiri;
- (b) Kumpatia Mwajiri ratiba ya kazi (*work programme*)ndani ya siku 7 tangu tarehe ya kusaini Mkataba huu ili kupata kibali cha Mwajiri.

IMESAINIWA NA KUWEKWA MHURI, KWA NIABA YA MAMLAKA YA ELIMU NA
MAFUNZO YA UFUNDI STADI, NA CHUO CHA UFUNDI STADI (NA HUDUMA) CHA
MPANDA

Jina: Tastrea Mariane Saini:



Wadhifa: HCUV na CHUO Tarehe: 21/03/2022

Mbele ya (Shahidi)

Jina: ERASmus ZUMBA Saini:



Wadhifa: MWAZI MU Tarehe: 21/03/2022

IMESAINIWA NA FUNDI

Jina: PASCAL-G KWIMBA

Mbele ya.

Wadhifa: FUNDI NKUMU

Saini:



Tarehe:

21/03/2022

Mbele ya (Shahidi)

Jina: JOHN CHISENGA

Saini:



Wadhifa: FUNDI NYAILI Tarehe:

21/03/2022